ASUMBI GIRLS HIGH SCHOOL

POST -MOCK 1

AUGUST/SEPTEMBER

2022

**MWONGOZO**

**102/ 2 KISWAHILI Karatasi ya Pili**

**LUGHA**

**Muda: Saa 2 ½**

**Jina…………………………………………Nambari ya Mtahiniwa……………………**

**Sahihi ya Mtahiniwa………………… Tarehe……………….………..**

**AGOSTI 2022**

**Maagizo**

a) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoaciwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali yote*
d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*
f) *Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.*
g) **Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee:**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| **1** | **15** | |
| **2** | **15** | |
| **3** | **40** | |
| **4** | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha utekeleze maagizo yafuatayo**

Utotoni niliamini kwamba kusoma ndiko ufunguo wa kila kitu ulimwenguni kwa jinsi kunavyoonekana kuwatoa watu katika uzuzu, ukata na ugonjwa: na kuweka kwenye maisha bora ya mwangaza wa kujua kusoma na kuandika, utajiri wa kuweza kuvaa hata suti ya vipande vitatu, na kuwa na afya ya kuonekana kwa kitambi. Hizo ni zamani zile ambapo shule ya vidudu haikuwa sharti la mtoto kukubaliwa katika darasa la kwanza. Mtoto angelisha au kusaidia kwa kazi za nyumbani mpaka kufika umri labda wa miaka kumi kisha, kufumba na kufumbua, afisa wa serikali angeonekana akishauriana na mzazi wa mtoto. Matokeo yangekuwa mtoto huyo kuanza safari ndefu ya kila siku, apate asipate chakula.

Mimi kwa upande wangu sikujali maisha pata-nenda shule, kosa – bado – nenda – shule. Sikujali kero za baridi kali wala karaha za vua la asubuhi. Kuanzia utotoni *niliwahusudu* wenzangu waliokuwa wakirauka kiasi cha kufikiriwa kuwa walilala kwa shati na kaptula zao, au kwa blauzi na skati na kaptula zao. Nilipendezwa na yunifomu zao nikatamani na hata kuapa kwamba siku moja nitavaa kama wao na kutembea kwa maringo kama wao. Zaidi nilitamani kufika walikokuwa wakienda na kufanya walivyokuwa wakifanya huko.

Penye nia hapakosi njia. Nia yangu ilidhihirika pale nilipojiunga na darasa la kwanza. Darasa la kwanza lilinisoma kisogo baada ya siku mbili tu. Nalo la pili likanipungia mkono baada ya juma moja. Miaka mitano baadaye nilikutana na kiunzi cha kwanza kwenye mtihani wa kitaifa wa chumba cha saba uliokuwa kifungua mlango wa kuingilia kidato cha kwanza.

Baada ya miaka minne nilikutana na mlango funge mwingine ambapo nilibisha na ukanifungukia kwa *kutia fora* katika mtihani wa kiwango cha elimu ya upili. Katika miaka miwili iliyofuatia nilijiunga na shule maarufu ya kitaifa siku hizo.

Masomo hayakuendelea kuwa mteremko kwangu kwani uchechefu wa karo na masurufu ulimaanisha kuwa siku nyingi nilikuwa nje ya kuta za darasa letu. Hata ivyo *nilijifunga masombo.*Hatimaye nilifunguliwa milango ya kuingia ndaki.

Baada ya kuhitimu kwa shahada ya kimsingi ya uzamili, kisha uzamifu au udaktari falsafa hatimaye, nilifanywa meneja kufikia leo. Hata nikiwa ukubwani bado ninazidi kusoma na kutafiti ili nisiote ukurutu wa akili.

Cheo na madaraka haya ya umeneja yamaanisha kila siku nivae suti kamili na shati nyeupe pe, ambayo shingoni imeambatanishwa na kipande maalumu cha kitambaa kinacholewalewa kifuani. Nijiangaliapo kiooni hujifananisha na mtu ambaye amejitia kitanzi shingoni.

Nina kitambi ambacho labda ni *taashira* ya utajiri. Hata hivyo ingawa mimi si tajiri mwenye sauti kubwa kiuchumi, ninaweza kujivunia elimu yangu iliyoniwezesha kujimudu kidogo maishani. Sasa nina shamba langu mwenyewe, nyumba yangu mwenyewe ambayo imejaa mali yangu mwenyewe. Nina redio yangu mwenyewe, rununu yangu mwenyewe na wanyama wangu mwenyewe.

Lakini mwenzangu ambaye zilimwishia ukingoni katika shule za nasari, hana elimu, pesa wala mahali pa kuzikiwa wakati mpira utakapomwia mwingi.

**MASWALI**

a) Eleza imani ya mwandishi kuhusu elimu. (alama 3)

kusoma ndiko ufunguo wa kila kitu
huwatoa watu katika ujinga, uzuzu, umaskini na ugonjwa
huwaweka watu kwenye maisha bora ya mwangaza
huwaweka watu kwenye utajiri

zozote 3

b) Taja dhiki zilizomkabili mwandishi alipokuwa shuleni ( alama 2)

-kukosa chakula
- baridi kali
- mvua a asubuhi
- ukosefu wa karo na masurufu mengine

Hoja 4x½ = 2

c) Onyesha uhusiano uliopo kati ya elimu, kazi na ukwasi kwa mujibu wa habari hii.

(alama 3)

d–elimu na kazi – mtu aliyeelimika aliweza kuajiriwa

- elimu na ukwasi – elimu humwezesha mtu kujimudu maishani ingawa si lazima awe tajri Hoja 2x1 = 2

e.Ukirejelea makala haya, fafanua msemo, ‘elimu ni bahari haina kikomo’ (alama 3)

Mwandishi ameelimika sana / amepata shahada mbalimbali na kufanywa meneja lakini anazidi kusoma na kufanya utafiti

Hoja kamili, alama 3

F. Hatima ya wale ambao hawakupata elimu ni ipi? (alama 2)

kutojimudu maishani
- kutojimudu kiakili

g. Badala ya maneno yafuatayo mwandishi angetumia msamiati gani? (alama 3)

i. Niliwahusudu - niliwaonea wivu / niliwapenda / niliwahusudu
ii. Nda - chuo kikuu / zutafindaki
iii. Taashira-dalili/ishaa

**UFUFISHO**

**a**

- Dhuluma kwa kwa mwanamke ni hali ya tangu jadi
- Elimu ya jadi ilimwandaa Kama chombo cha mume
- Taasubi ya kiume
- Mwanamke Kama msihiri na mgaga.
- kupuuzwa na kutukanwa hadharani
- Demokrasia ilimfungia nje. Alama 6

b)

- Matokeo ya elimu ya kisasa
- mwanamke wa enzi mpya

- mwanake kujiami na kujiendeleza
- vipaji katika Nyanja mbalimbali
- Kikwazo cha itikadi na mila za kiasili
- wadumishaji wa dhuluma wasalimu amri
- mwanamke anayeongoza maisha yake
- Hadhi ya mwanamke kukua

alama 8

**6+8+1 ut-hijai-sarufi-ziada**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

a) Tofautisha Irabu /u/ na /o/ (Alama 2)

/u/ juu

/o/ wastani

b) Tunga sentensi ili kubaini matumizi ya neno vibaya katika sentensi kama;

kielezi na kivumishi (Alama 2)

kielezi- mfano; Ameandika vibaya.

kivumishi – mfano; Viatu vibaya vimetupwa

c) Yakinisha sentensi ifuatayo.

Nisipomwona sitamlipa pesa zake. (Alama 1)

Nikimwona nitamlipa pesa zake.

d) Tumia kivumishi cha 'a' unganifu katika sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya A-WA. (Alama 2)

mfano ; Mwalimu wa Kiswahili amewasili.

e) Tunga sentensi ili kutofautisha vitenzi vifuatavyo.

i) ni (Alama 1)

Yeye ni mwalimu.

ii) yamekuwa (Alama 1)

Yeye alikuwa mwalimu

f) Tunga sentensi ili kubaini; (Alama 2)

kivumishi cha idadi jumla

mfano; Watoto wachache/ tele/ wengi waliwasili.

kivumishi cha idadi kamili

Watoto wawili/watatu/mmoja/ wanne nk wamewasili.

lazima apigie mstari

g) Toa maana mbili ya sentensi hii

Nionyeshe vile nitakavyobeba. (Alama 2)

jinsi

vitu vya kubeba

h) Kanusha sentensi ifuatayo kwa njia mbili .

Wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi. (Alama 2)

a Wachezaji hawakuwa wanafanya mazoezi.

b Wachezaji walikuwa hawafanyi mazoezi.

i) Andika katika usemi wa taarifa.

"Tutakwenda kanisani kesho kutwa." Kame alisema. (Alama 2)

Kame alisema kuwa wangeenda kanisani siku ya pili iliyofuata siku hiyo.

j) Changanua sentensi hii kwa kutumia kielezo jedwali. (Alama 4)

"Mshale huu mrefu umevunjika mara mbili

| S√1 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | | KT√1 | |
| N | V | V | T | E√1 |
| mshale | huu | mrefu | umevunjika | Mara mbili√1 |

k) Tunga sentensi mbili tofauti ili kudhihirisha matumizi ya 'mshazari' (Alama 2)

**a)** yaweza kutumiwa kuonyesha kumbukumbu. KA/45/4M

**b)** kuonyesha maneno fulani yana maana sawa. Mwana/ mtoto wa shangazi ni mzuri.

**c)** Hutumiwa badala ya **au.**Bw/Bi/Dkt/Prof Vitabu/kalamu/chaki ni muhimu.

**d)** Hutumika katika tarehe, mwezi na mwaka. 13/2/2013

l) Unganisha sentensi hii kwa kutumia kirejeshi 'O' Kucha zake ni ndefu. Kucha zimekatwa. (Alama 1)

Kucha zake zilizokuwa ndefu zimekatwa.

m) Eleza matumizi ya 'Ki' katika sentensi

Ukirusha kipira kitapotea (Alama 3)

Ukirusha _ya masharti

Kipira _udogo

Kitapotea _upatanisho wa ngeli

n) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoonyeshwa. (Alama 2)

La _lishana al. 1 (hakiki sentensi. Za mtahiniwa )

Pa _pasha al. 1 (hakiki sentensi. Za mtahiniwa)

o) Andika neno lenye kiyeyusho. (Alama 2)

/W/ waya /Y/ yeye

p) Andika kwa wingi

Mtoto yuyu huyu ndiye aliyeiba nguo yangu. (Alama 1)

Watoto wawa hawa ndio walioiba nguo zetu

q) Unda sentensi yenye vijenzi vifuatavyo vya kisarufi.

Kiwakilishi + kivumishi + kitenzi + kielezi (Alama 1)

mfano; Mimi mfupi kupita kiasi/ Yule mrefu amekimbia sana

r) Akifisha sentensi ifuatayo ;

Bw. Juma alimwambia bibi yake, 'Nitakutuza ukiendelea kutenda mazuri.' (Alama 2)

s. Tunga sentensi mbili ili kuonyesha tofauti kati ya maneno yafuatayo; (alama 2)

i. kua

zidi kwa umri- mfano- Mtoto amekua haraka hadi ameenda shuleni.

ii. kuwa

hali- Alikuwa mgonjwa.

t. Tunga sentensi moja yenye virai viuatavyo. (alama 2)

RN (nomino, kivumishi kielezi), RT (kitenzi, nomino)

Mfano

Kaka mzuri sana amenunua matunda.

u. Andika katika udogo. Kitabu cha mtu huyo kimeletwa na mwanafunzi wake. (alama 1)

Kijitabu cha kijitu hicho kimeletwa na kijanafunzi chake.

**4. <u>ISIMU JAMII</u>**

a) _Tatizo la matamshi ya sauti

/d/, /b/, /l/, /sh/’ /h/. (al. 2)

_Athari za lugha ya kwanza.

b) -Athari za lugha ya kwanza

-Ujuzi wa lugha nyingi za mzungumzaji

-kutofahamu kanuni za sarufi

-kutafsiri lugha ya mama katika Kiswahili

-upungufu wa viungo vya kutamkia kama meno, ulimi

-ukosefu wa baadhi ya sauti za Kiswahili katika lugha ya asili

-kuzungumza kwa haraka

-ugonjwa

-kutoimudu lugha vilivyo

-kurithishwa lugha isiyo sanifu na matamshi mabaya aidha na mwalimu au wazazi.